## *Usoni wako ni siku yako kuu zaidi na tishio kubwa kwa maadui wako*

Tunakuja kutoka kwa siku yetu kuu, tuko kwa siku yetu kuu, ama tuna elekea kwa siku kuu yetu, na ukweli ni- ni uamuzi wetu. Mkristo amebarikiwa na ufahamu kwamba hata akiwa ndani ya hatari ya kifo, siku yetu kuu bado iko mbele yetu.

Weka mawazoni mwako kuwa Mungu hata waruhusu maadui wetu watushinde sisi. Anampango ambao unahusisha ushindi juu ya mauti, kuzimu na kaburi. Mpango huu wa ushindi pia unahusisha hali zako za sasa na matukio ya maisha. Usoni mwako umo na siku yako kuu zaidi na una tishio kubwa kwa maudui zako.

*Ombi la leo:*
Tumaini langu ni ndani Yako Bwana. Mbio sio ya wale wepesi wala vita sio ya wenye nguvu, lakini Wewe, Ewe Bwana, humuinua na kuweka mwingine kama inavyo kupendeza Wewe. Nipe ushindi katika changa moto zote na uniwezesha kuwashinda maadui wangu kupitia kwa Neno na Roho wako.

*Masomo ya leo:*
Yeremia 29:11; maana ninayajua mawazo ninayo wawazia nyinyi, asema BWANA, ni mawazo ya amani wala sio ya mabaya, kuwapa ninyi tumaini siku zenu za mwisho.

1 Wakorintho 2:9; Lakini, ni kama yasemavyo Maandiko Matakatifu: "Mambo ambayo jicho halijapata kuyaona wala sikio kuyasikia, mambo ambayo binadamu hajapata kuyafikiria moyoni, hayo ndiyo Mungu aliyowatayarishia wale wampendao."

2 Wathesolenike 1:6; Mungu atafanya jambo la haki: atawalipa mateso wale wanaowatesa ninyi,

Ufunuo wa Yohana 20:10; Ibilisi, aliyekuwa anawapotosha, akatupwa ndani ya ziwa linalowaka moto wa kiberiti, walimo yule mnyama na yule nabii wa uongo, nao watateswa mchana na usiku, milele na milele.

## *Upendo ambao ni upendo unalazimu kuonyeshwa*

“kwa maana jinsi hii, Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanaye ….” Upendo hulazimisha kuonyeshwa na upendo sana sana

hudhibitishwa kupitia kitendo cha kutoa. Yesu akasema, kama unanipenda, utatii amri zangu. Baadaye, akamuuliza Petro, “unanipenda?” alipojibu kwa kukubali, Yesu akamjibu kwa kumtia moyo Petro kufanya kitu cha kuchukua hatua na kuonyesha upendo ule kwa kuwalisha kondoo Wake.

Mtume Yohana alisema, mtu yeyote ambaye amemiliki mema ya dunia na amuone jirani yake akiwa na hitaji na asiwe na huruma za kumfanya achukuwe mali yake ampe jirani yake, basi ni nini kinaweza kufanya mtu yeyote awazie kuwa upendo wa Mungu uko ndani ya huyu mtu? Unaona, upendo ambao ni upendo unahitaji kuonyeshwa.

## *Ombi la leo;*

Mungu, ninakupenda na nina tamani kukuonyesha Wewe upendo wangu kwa yale ninatenda kwako Wewe na wengine kwa jina Lako. Nipe uhuru kuonyesha upendo wangu kwa njia pana ili nifanyike Mkono Wako ulionyoshwa duniani.

## *Masomo ya leo:*

Yohana 3:16; Maana Mungu aliupenda ulimwengu hivi hata akamtoa Mwana wake wa pekee, ili kila amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.

1 Yohana 3:17; Basi, mtu akiwa na mali za hapa duniani, halafu akamwona ndugu yake ana shida, lakini akawa na moyo mgumu bila kumwonea huruma, anawezaje kusema kwamba anampenda Mungu?

Yohana 14:15; "Mkinipenda mtazishika amri zangu.

Luka 6 :32; Na ikiwa mnawapenda tu wale wanaowapenda ninyi, je, mtapata tuzo gani? Hakuna! Kwa maana hata wenye dhambi huwapenda wale wanaowapenda wao.

# ***Kuwa tayari wakati wote kwa Neno jipya la Mungu***

Siku moja Mungu alimunenea Ibrahimu wazi wazi na kumwambia achukue safari na amtoe dhabihu mwanaye Isaka juu ya mlima Moria. Hapo hapo, Ibrahimu akatii neno la Mungu na akasafiri siku tatu kabla kukwea milma na kujenga madhababu ya Bwana. Hapo, Ibrahimu akamfunga mwanaye na kumwadaa kama dhabihu ndio amuue kwa kutii neno la Mungu lilokuwa wazi. Wakati Ibrahimu alipoinua kisu

chake amuchinje mwanaye wa kiume, Malaika wa Bwana akanena na kusema, “usimuumize huyo mtoto.”

Ni lipi kati ya maneno haya mawili lilitoka kwa Mungu? Yote mawili! Kama Ibrahimu hangetii neno lolote kati ya haya, ingekuwa jambo mbaya. Kama Ibrahimu, lazima tulitii neno la Mungu na kila wakati tuwe tayari kwa neno jipya pia. Wakati mwingine tunatembea hadi mwisho ili tufikie mwisho wa barabara na wakati mwingine Mungu anatutuma hadi mwisho ili tupate msaada iliyoko barabarani.

## *Ombi la leo*

Mpenzi Bwana, Naamua kukubali Neno Lako kama mamlaka ya mwisho maishani mwangu. Nena kwangu na udhibitihe Neno Lako kwangu. Pia Baba, kama wataka, ninee neno jipya kwa maisha yangu. Nitaweka moyo wangu wazi na masikio yangu yakingojea sauti Yako.

## *Masomo ya leo*

Mwanzo 22:11-14; ndipo malaika wa Bwana akamuita toka mbinguni akasema, “ Ibrahimu! Iburahimu!” naye akasema, “mimi hapa.” Akasema, “ usimnyoshee kijana mkono wako, wala usimtendee neno; kwa maana sasa ninajua ya kuwa unamcha Mungu, iwapo hukunizuilia mwanao, mwanao wa pekee.” Ibrahimu akainua macho yake, akaangalia, na tazama, kondoo mume yuko nyuma yake, amenaswa pembe zake katika kichaka. Basi, Ibrahimu akaenda akamtwaa huyo kondoo, akamtoa kuwa sadaka ya kuteketezwa badala ya mwanawe. Ibrahimu akapaite mahali hapo Yehova – yire, kama watu wasemavyo hata leo, katika mlima wa Bwana itapatikana.

# *Usalama, ulinzi, na nguvu ziko katika undani na upana, sio katika urefu*

Umewahi weka mawe kupanda juu, moja juu ya lingine, hadi yakakosa kuwa imara na kutikiswa kudogo kukuyafanya yakaanguka? Hii ni picha ya mtu ambaye anatafuta kupanda juu na juu zaidi katika jitihada zake za kibinafsi. Inafananishwa na mti ambao hukua kwa haraka na kuwa mrefu, ukielekea mbinguni na kufunika jua, mara nyingi ukiwa mrefu zaidi na kufunika miti iliyo karibu, bila kutumia muda na nguvu zinazofaa ili kusukuma mizizi yake ndani ya undongo na kutafuta nguvu zake kwa njia iliyo panuka ili kuishikilia kwa usalama. Upepo mdogo unaweza kusababisha mti ule kuanguka.

Amua sasa kwamba utatumia muda kiasi kizuri kukufanya kwanza uzame ndani ya Kristo na upanuke katika mambo ya Mungu kabla

upande juu zaidi hadi ushindwe kujishikilia, ufanyike dhaifu na mwishowe uporomoke.

*Ombi la leo*

Mungu, niwezeshe nitembee siku ya leo, sio kwa ufahamu na uwezo wangu, lakini kwa neema na nguvu zako ambazo huishi ndani yangu. Leo, nakuomba Uupe msingi wa imani yangu nguvu ili niweze kushinda majaribu ya uoga na niwe kizingiti imara katika ufalme Wako.

*Masomo ya leo*

Luka mtakatifu 8:11-14; Basi, maana ya mfano huu ni hii: mbegu ni neno la Mungu. Zile zilizoanguka njiani zinaonyesha watu wale wanaosikia lile neno, halafu Ibilisi akaja na kuliondoa mioyoni mwao wasije wakaamini na hivyo wakaokoka.Zile zilizoanguka penye mawe zinaonyesha watu wale ambao wanaposikia juu ya lile neno hulipokea kwa furaha. Hata hivyo, kama zile mbegu, watu hao hawana mizizi maana husadiki kwa kitambo tu, na wanapojaribiwa hukata tamaa.Zile zilizoanguka kwenye miti ya miiba ni watu wale wanaosikia lile neno, lakini muda si muda, wanapokwenda zao, husongwa na wasiwasi, mali na anasa za maisha, na hawazai matunda yakakomaa.

## ***Sababu zinazomfanya mtu aende kanisani zinadhibitisha mtu ataenda kanisa wapi***

Umesha wahi kufanya uchunguzi ni kwa nini wewe huenda kanisani? Wewe huenda kanisani kujazwa na kusisimuliwa? Unaenda kwa sababu ya uhusiano wa kiroho ama wa kibashasha? Unaenda kufanya urafiki na kuwa na ushirika na waumini wengine? Unaenda kwa vile unampenda mchungaji na ujumbe wake ama unapenda jengo na mambo mengine? Orodha ya visababu kwa nini unaenda kanisani yaweza kuendelea.

Sababu zinazomfanya mtuu aende kanisani zinadhibitisha mtu ataenda kanisa wapi. Muulize Mungu kama sababu zako zinatosha, na kama hazitoshi, kabla ubadilishe makanisa, tafuta kwanza ni sababu gani kabla haujaenda.

*Ombi la leo*

Ahsante Mungu, kwa kunifanya sehemu ya mwili wa Kristo na kuniweka ndani ya kanisa nzuri. Fanya mahitaji na shauku langu jinsi unataka ziwe ili niungane na wengine wenye maono saiwa na tufanye utofauti ndani ya ulimwengu huu.

*Masomo ya leo*

Luka Mtakatifu 4:16; Basi, Yesu alikwenda Nazareti, mahali alipolelewa, na siku ya Sabato, aliingia katika sunagogi, kama ilivyokuwa desturi yake. Akasimama ili asome Maandiko Matakatifu kwa sauti.

Isaya 55:1-3; Haya, kila aonaye kiu, njoni majini, naye asiye na fedha; njoni nunueni mle, naam, njoni, nunueni diva ina maziwa, bila fedha na bila dhamani. Kwani kutoa fedha kwa ajili ya kitu ambacho si chakula? Na mapato yenu kwa kitu kisicho shibisha? Nisikilizeni kwa bidii, mle kilicho chema, na kujifurahisha nafsi zenu kwa unono. Tegeni masikio yenu, na kunijia; sikieni na nafsi zenu zitaishi; nami nitafanya nanyi agano la milele, naam, rehema za Daudi zilizo imara.

## *Kanisa lina utaratibu wa vile litafanya kazi*

Tunaweza kosa hekima kuwazia kuwa twaweza ajiliwa na kampuni yoyote kama wafanyi kazi wapya na kisha tuasi kinyume na utaratibu wa sheria na kanuni zao na bado tutarajie kuwa na shughuli yenye faida. Uasi dhidi ya utawala wa halali ulioko mara nyingi husababisha shida kubwa zaidi na hutumika kututenga sisi huku ukigandamiza wengine waliotuzunguka wenye mawazo tofauti. Twaweza fanya bora zaidi kuchunguza mahali unakokusudia kuandikwa kazi kuhakikisha tutajitoa na kujitolea kwa utaratibu wa uongozi ulioko kabla ya kukubali kazi na kampuni yeyote.

Makanisa, ni tofauti. Kuna makanisa mengi katika msingi yao wanaoamini Yesu Kristo kuwa njia ya pekee ya mbinguni, lakini mitindo yao ya uongozi huenda ikawa na utofauti mkubwa. Kujitolea kwa mamlaka ya kanisa yanayotawala ni mapenzi ya Mungu kwa kila muumini ambaye anaendelea katika ushirika wa kinisa hilo. Hii inahifadhi umoja katika imani na uendelezaji wa nje. Vile kanisa lilivyo pangika ndivyo linalo uwezo wa kutenda kazi.

*Ombi la leo*

Baba, nisaidie niwe mtumishi mwenye hekima katika nyumba Yako. Nipe roho wa kuelewa na unyenyekevu katika kanisa ambalo umeniweka. Natamani niwe wa baraka na sio shida katika mamlaka yangu ya kiroho

*Masomo ya leo*

Waebrania 13:17; Watiini viongozi wenu na kushika amri zao; wao huchunga roho zenu usiku na mchana, na watatoa ripoti ya utumishi

wao mbele ya Mungu. Kama mkiwatii watafanya kazi zao kwa furaha, la sivyo, watazifanya kwa huzuni, na hiyo haitakuwa na faida kwenu

Yakobo 5:9; Ndugu zangu, msinung`unikiane ninyi kwa ninyi msije mkahukumiwa na Mungu. Hakimu yu karibu, tayari kuingia.

## ***Kuketi kanisani hakutakufanya uwe Mkristo zaidi ya vile kuketi kwenye gereji kutafanya uwe gari***

Umilele tu ndio utakaoamua ni watu wangapi wameketi katika viti vya makanisa duniani ambao walitenda na walimiliki katika ufahamu wa wokovu wa Yesu Kristo.Baadhi ya uwongo mkubwa ambao shetani ameweka kwa wengi ni kwamba wakisha kwenda kanisani imewatosha kuingia mbinguni. Ukweli ni kwamba, Mungu anajua hali zilizofichika za mioyo yetu na ni mioyo yetu tu (wala sio wapi ama kama tunakwenda makinisani) ambayo ina amua umilele wetu.

Kwa ukweli, kanisa ni la ulimwengu wetu na umilele wote. Tunafanyika washirika wa "kanisa" kwa kukubali na kumpokea Yesu Kristo kama Bwana na Mwokozi. Je, wewe kweli ni Mkristo ama tu umeshikilia sehemu? Muulize Yesu aingie maishani mwako leo na ataandika jina lako katika kitabu cha uzima!

### *Ombi la leo*

Baba, natamani kuwa Mkristo wa kweli. Nakuomba unisamehe dhambi zangu na uingie ndani ya maisha yangu. Niongoze katika njia za haki kwa sababu ya jina Lako. Naamini, moyo wangu umebadilishwa, na mimi ni Mkristo!

### *Masomo ya leo*

Matendo ya Mitume 11:26; Alipompata, alimleta Antiokia. Nao wote wawili walikaa na lile kanisa kwa mwaka wote mzima wakifundisha kundi kubwa la watu. Huko Antiokia, ndiko, kwa mara ya kwanza, wafuasi waliitwa Wakristo.

Yakobo 1:22; Msijidanganye wenyewe kwa kusikiliza tu neno lake, bali litekelezeni kwa vitendo.

## ***Kusoma maagizo ya upishi sio sawa na kupika keki yenyewe.***

Tunaweza kuwa na makusudi mengi maishani, hata kuweza kuyaandika chini katika oradha ya mambo yetu ya kufanya kwa siku hiyo, lakini hayamaanishi chochote na hayatekelezi chochote hadi tuweke matendo. Katika mtembeo wetu wa Kikristo, tumepewa maagizo ya wokovu na kuishi maisha ya kiungu. Kusoma tu kuyahusu, haitakufanya maankuli yako ya Kiroho ya jioni yawe yameiva. Tunatarajiwa kupokea halafu tutende kadiri ya Neno la Mungu lili tuweze kuvuna ahadi za Mungu. Unapojua la kufanya kulingana na Neno la Mungu, hauna mwingine wa kulaumu ila wewe mwenyewe unapokosa kuitikia na kutii kwa sababu ni kutii kwako ambako kutaleta miujiza unayoihitaji.

Jitie moyo kwa kufanya kazi kidogo na kuchanganya na imani na Neno la Mungu leo kisha uangalie maisha yako yakiinuka juu, yakionja utajiri, na yakifanyika ya muhimu kuliko hapo awali.

### *Ombi la leo*

Baba, nakushukuru kwa Neno Lako la ajabu. Ni maagizo ya kunawiri, furaha, na maisha yaliyo na afya kwako. Nisaidie leo, sio tu kusoma lakini kutenda utukufu Wako!

### *Maandiko ya leo*

Yakobo 4:!7; Basi, mtu ambaye hafanyi lile jambo jema analojua kwamba anapaswa kulifanya, anatenda dhambi.

Waebrania 4:2; Maana Habari Njema imehubiriwa kwetu kama vile ilivyohubiriwa kwa hao watu wa kale. Lakini ujumbe huo haukuwafaa chochote, maana waliusikia lakini hawakuupokea kwa imani.

Yakobo 2:26; Basi, kama vile mwili bila roho umekufa, vivyo hivyo imani bila matendo imekufa.

## ***Tofauti ya mwito na mzigo***

Mwito ni mwaliko wa kuja na kujiandaa kimaisha kwenye huduma katika eneo Fulani la huduma. Wengi wameitwa lakini wachache wameteuliwa. Sababu ya kuwa wengi wameitwa na wachache wameteuliwa, ni kwa vile wachache ndio wanao tumia nguvu zao na muda unao hitajika katika kujiandaa. Mwito unahitajikana kukaa milele. Hata hivyo, mzigo unaweza kuwa ni matokeo ya Mungu akihitaji kitu kitendwe na pasipo kupata mtu anayepatikana, anakuchagua wewe kubeba mzigo.mizigo, sio kama mwito, mara nyingi inaondolewa

kulingana na wakati ama jukumu likimalizika. Shinda moja ni kuwa wakati mwingi tunaweza kosa kujua tunapokea mwito(ambao unahitaji matayarisho mengi)ama tumepewa mzigo( ambao unahitaji kuangaliwa haraka kihuduma) hadi tunapomuuliza Mungu.hakikisha kuwa ni mwito ama ni mzigo kutoka kwa Mungu kabla ya kujitolea maishani.

*Ombi la leo*

Mungu, nisaidie kuendelea kutambua mizigo mipya katika maisha yangu na kutenda kazi katika mwito uliouweka ndani ya maisha yangu. Nataka kufa nikitenda ulichoniita nitende. Nifanye niwe bora kwa kile ulicho niitia kutenda. Nipe mizigo uliyokusudia ni ibebe na uwache nitumikie ufalme wako milele.

*Maandiko ya leo;*

Mathayo 22:14; Yesu akamaliza kwa kusema, "Wengi wamealikwa, lakini wachache wameteuliwa."

2 Peter 1:10; Kwa hiyo basi, ndugu zangu, fanyeni bidii zaidi kuufanya huo wito wenu mlioitiwa na Mungu uwe jambo la kudumu katika maisha yenu; kama mkiishi namna hiyo hamtaanguka kamwe.

Wagalatia 6:2;Saidianeni kubeba mizigo yenu na hivyo mtatimiza sheria ya Kristo.

## ***Ni makosa kuwa na matarajio bila kuchunguza viwango ama hatimu zinazo weza kuzuia kushiriki***

Je umeshawahi kuwa na msisimuko kwa sababu ya jambo unalotaka kulitenda? Halafu ukamwalika mtu mwingine ama watu wengi wengine kuhusika pamoja na wewe. Walikuwa na matarajio kwa sababu uliwachorea maono hayo mazuri ya vile kungalikuwa. Pengine ilikuwa ni mapumziko, ama safari ya umeshanali, ama sherehe ya kuzaliwa, ambayo haukuangalia kwa undani. Ilipokaribia wakati wa wewe kutoa, ilionekana kuwa ya gharama, pengine ya hatari, tarehe hazikufaa, ama haikuwa safari yako, lakini mtu mwingine ndiye alikuwa amesimamia na ukapuuza kupewa idhini yao. Pengine, haujapitia jambo kama hili, lakini mara kwa mara, inatendeka kwa watu wasio na hatia na wanao maanisha wema. Tia maanani ya kwamba ni vibaya kumtunga mtu miimba ya maono na kumpa matarajio hadi uwe na hakikisho ya kwamba utafaulu.

*Ombi la leo:*

Baba, nisaidie kuwa na busara, hekima na subira. Nipe picha kubwa ya kuelewa ili nisiongoze watu mahali na kisha niwaache kama wamepotea. Pahali nilipo na udhaifu, najua wewe uko na nguvu na hivyo, nakutegemea wewe, unisaidie kupanga bali pahali nisipo ona.

*Maandiko ya leo*

Mithali 29:18;  pasipo maono, watu huwacha kujizuia; Bali ana heri mtu yule aishikaye sheria.

Mithali 14:15; Mjinga huamini kila neno; Mbali mwenye busara huangalia sana aendavyo.

Luka Mtakatifu 14:28; Kwa maana, ni nani miongoni mwenu ambaye akitaka kujenga mnara hataketi kwanza akadirie gharama zake ili ajue kama ana kiasi cha kutosha cha kumalizia?

## *Kuweka ukweli kwako binafsi sio uwongo*

Mfalme Hezekia,{ 2 Wafalme 20, Isaya 39} , akafanya makosa ya mauti kwa kuonyesha wageni wa Babiloni hazina zao zote nyumbani mwao. Aliwaonyesha fedha, dhahabu, viungo vya chakula, manukato, silaha zake zote, na kila kitu chake cha dhamana. Nabii Isaya, akamkemea mfalme Hezekia kwa kitendo chake cha upumbavu. Kwa sababu Hezekia alikuwa amejaribu kuwaonyesha maadui zake kila kitu, kwa hivyo sasa, kwa Neno la Bwana, imekusudika mwishowe kupoteza vyote.

Yesu, akanena katika Mathayo saba ya kwamba msiwape nguruwe lulu zenu kwa sababu hawatashukuru ila kuzikanyaga na kugeuka kuja kinyume nanyi. Muwe waangalifu na wale mnao shiriki mambo yenu ya dhamana. Lindeni kile Mungu alicho wapa kisitumiwe vibaya, kuharibiwa, ama kutumiwa kama ushahidi ama fursa kinyume na nyinyi

*Ombi la leo*

Ewe Mungu, nifunze kuwa makini na kile nishirikicho na wale ninao shiriki nao. Nisaidie nisitegwe katika mitego ya upumbavu kwa kufungua kinywa changu na kusema yote kwa wale ninajua wanatafuta kuniangamiza. Nifanye niwe na hekima Bwana. Amina.

*Maandiko ya leo:*

Mithali 13:3;  yeye alindaye kinywa chake hulinda nafsi yake; Mbali afunguaye kinywa chake atapata uharibifu.

Yohana Mtakatifu 8:6 ; Walisema hivyo kumjaribu, wapate kisa cha kumshtaki. Lakini Yesu akainama chini, akaandika ardhini kwa kidole.

Mithali 26:4,5;  usimjibu mpumbavu sawasawa na upumbavu wake; usije uka fanana naye. Umjibu mpumbavu sawasawa na upumbavu wake asije akawa mwenye hekima machoni pake.

## ***Kanisa sio hifadhi ya kuweka kumbukumbu ya kile Mungu alitenda lakini ni hifadhi ya joto ya kuzaa kile Mungu angelipenda kutenda***

Tunaelezwa, kuna aina mbili za watu… wale wanao soma historia na watengenezaji wa historia! hii huenda ikawa ukweli kuhusu kanisa. Neno la Mungu hutupatia ukweli, kanuni, na mfumo ambao tunahitaji kutumia kuendeleza na kuboresha ufalme wa Bwana.  Ikiwa yale tu kanisa imeshawahi tekeleza ni kufunza watu yale Mungu alifanya, na kamwe washirika hawahamasishwi kuhusika na kile Mungu angetaka kutenda, basi kanisa litakuwa halina nguvu.

Ukristo ni zaidi ya kujifunza kuhusu Mungu pekee na yale alitaka kufanya siku zilizo pita. Inahusu pia kujua kwa kibinafsi na kujihusisha na kile Anataka kutenda siku ya leo. Lazima tuhifadhi Neno la Mungu na ni lazima pia tulitumikie!

### *Ombi la leo*

Mungu, nakushukuru kwa kuniumba ili nitengeneze historia. Nataka kuwa muhusika mwenye bidii katika mpango Wako wa maisha yangu. Tafadhali nipe nguvu, uwezo, na shauku la kuendeleza na kutengeneza ufalme Wako. Asante kwa siku zangu zijazo Mungu.

### *Maandiko ya leo*

Yakobo 1:22; Msijidanganye wenyewe kwa kusikiliza tu neno lake, bali litekelezeni kwa vitendo.

Warumi 4:23-24;Jambo hili linatuhusu sisi pia ambao tunamwamini Mungu aliyemfufua Yesu, Bwana wetu, kutoka wafu.Inaposemwa, "Alimkubali," haisemwi kwa ajili yake mwenyewe tu.

Yakobo 2:20; Mpumbavu wee! Je, wataka kuonyeshwa kwamba imani bila matendo imekufa?

## ***Utakalojuta pekee unapofika mbinguni ni kuwa haukuenda awali***

Bibilia inaonyesha kuwa Mungu aliumba mbingu ikipendeza sana hivi kwamba hatuwezi tukawazia ukuu wa staajabu hili. Hebu jaribu kuwazia ujuzi wakupendeza namna gani tutakaopata, barabara za dhahabu, hakuna uchungu, hakuna machozi, hakuna dhambi… hautachoka wala kuwa na njaa, na hali ya hewa itakuwa ya kupendeza. Mungu alisema hata itakuwa nzuri kuliko tunavyoweza kuwazia.

Niamini, asilimia mia moja ya watu walioenda kabla yetu wanaishi vyema kuliko sisi na, naamini kama wangeachwa wajiamulie, wangeamua kubaki pale walipo. Kwa muumini anayepumua mara yake ya mwisho hapa duniani, tunaweza kuhakikishiwa kwamba siku kuu yao bado iko mbele.

### *Ombi la leo*

Asante Mungu kwa siku nzuri namna hii za usoni. Nina sisimka kuhusu umilele. Baba, Neno Lako linaniambia nijishughulishe na mambo ya kupanua Ufalme Wako hadi uje. Najitolea kufanya yote niwezayo kujenga ufalme Wako hapa duniani. Nionyeshe jinsi ya kuwa msimamizi mzuri wa wakati wangu duniani na unipe mtazamo wako wa umilele kuhusu maisha yangu.

### *Maandiko ya leo*

1 wakorintho 2:9; Lakini, ni kama yasemavyo Maandiko Matakatifu: "Mambo ambayo jicho halijapata kuyaona wala sikio kuyasikia, mambo ambayo binadamu hajapata kuyafikiria moyoni, hayo ndiyo Mungu aliyowatayarishia wale wampendao."

1 Petro 1:4; na hivyo tunatazamia kupata baraka zile ambazo Mungu aliwawekea watu wake. Mungu amewawekeeni baraka hizo mbinguni ambako haziwezi kuoza au kuharibika au kufifia.

Ufunuo 14:13; Kisha nikasikia sauti kutoka mbinguni ikisema, "Andika! Heri watu ambao tangu sasa wanakufa wakiwa wameungana na Bwana." Naye Roho asema, "Naam! Watapumzika kutoka taabu zao; maana matunda ya jasho lao yatawafuata."

Ufunuo 19:1; Kisha nikaona mlima Sioni, na Mwanakondoo amesimama juu yake; pamoja naye walikuwa watu mia moja arobaini na nne elfu ambao juu ya paji za nyuso zao walikuwa wameandikwa jina la Mwanakondoo na jina la Baba yake.

## *Msemo mgumu ni kile kitu tu ambacho hufanyi wakati huu*

Siku moja Yesu alikuwa akinenea kundi la watu na akawaambia, ili waweze kumfuata, itawabidi wawe kama yeye na wajikane. Wengine katika kundi wakanena na kutangaza kuwa Yesu alikuwa anawaamuru wafuasi wake mambo mengi zaidi. Kwa majibu yake ambayo hayakuwa na majuto, wengine wao wakajiondoa kutoka kwa kundi la kumfuata Yesu, wakitangaza kuwa ilikuwa vigumu sana.

Ninini kilicho kigumu kuhusu kumfuata Yesu? Chochote usichotaka kotoa. Inaweza kuwa ni fungu la kumi,kushuhudia, kunyenyekea kwa uongozi ambao umeteuliwa na Mungu, msamaha, ama kuwapenda maadui wako. Msemo mgumu ni kile kitu pekee ambacho hufanyi kwa wakati huu. Wengine katika kikundi siku hiyo walijitambulisha na matakwa ya Yesu na kuamua kile alichosema kuwa ndicho mkate wa uzima. Ni chaguo lipi kwako, Msemo mgumu ama mkate wa uzima?

### *Ombi la leo:*

Baba, naamini Neno Lako ni kuu kuliko hali zangu, hisia zangu, na mapenzi yangu. Nachagua kukubali Neno Lako kama suluhisho rahisi katika ugumu wa maisha. Nafanya uamuzi dhabiti kukumbatia mambo haya ungepende nifanye na sijakuwa nikifanya. Nisaidie, Bwana, nisikimbie na kusanyiko lakini kukubali Neno Lako kama mkate wangu wa kila siku.

### *Maandiko ya leo*

Yohana 6:60-61, 66-68; Basi, wengi wa wafuasi wake waliposikia hayo, wakasema, "Haya ni mambo magumu! Nani awezaye kuyasikiliza?" Yesu alijua bila kuambiwa na mtu kwamba wanafunzi wake walikuwa wananung`unika juu ya jambo hilo, akawauliza, "Je, jambo hili linawafanya muwe na mashaka? Kutokana na hayo, wengi wa wafuasi wake walirudi nyuma wasiandamane naye tena. Basi, Yesu akawauliza wale kumi na wawili, "Je, nanyi pia mwataka kwenda zenu?" Simoni Petro akamjibu, "Bwana, tutakwenda kwa nani? Wewe unayo maneno yaletayo uzima wa milele.

## *Je, ni wewe Yesu, basi niulize nitende jambo nisiloweza kufanya bila muujiza kutoka kwako*

Ikiwa yale yote unayotekeleza maishani ni yale tu unayoweza labda Mungu hafanyi mambo mengi maishani mwako. Katika Mathayo 14, Petro akumuuliza Yesu, “je, ni wewe… niamuru mimi…” kutenda kitu ambacho siwezi kutenda mwenyewe. Baadaye, tunamuona Petro akitembea juu ya maji.

Mungu anatafuta watu wa kawaida ambao watamuruhusu aenende katika maisha yao kupita uwezo wao kufanya mambo yasiyo kuwa ya kawaida. Koroga imani yako na usitishike wakati Mungu anakuongoza kutenda kuzidi uwezo wako. Aliye kuita atakuimarisha na aliyekuteua, atakutwalia.

### *Ombi la leo*

Mungu, nataka kuwa mkuu katika ukawaida wangu, kuishi maisha yangu katika kutwaliwa kwangu kwa kawaida, nikitendeza  kazi vipawa vyangu na karama zangu kutekeleza mapenzi Yako. Hata hivyo, Baba, pia nataka kuona miujiza, mambo zaidi ya uweza wangu ambayo yaweza kutekelezwa kwa imani yangu na neema yako. Nakupa maisha yangu. Tembea kupitia kwangu mimi.

### *Maandiko ya leo*

Mathayo mtakatifu 14:28; Petro akamwambia, "Bwana, ikiwa ni wewe kweli, amuru nitembee juu ya maji nije kwako."

Danieli 11:32; ….lakini watu wamjuao Mungu wao watakuwa hodari, na kutenda mambo makuu

Matendo ya mitume 19:11; Mungu alifanya miujiza ya ajabu kwa mikono ya Paulo.

Isaya 40:31; bali wao wamgojeao Bwana, watapata nguvu mpya, watapanda juu kwa mbawa kama tai, watapiga mbio, wala hawatachoka, watakwenda kwa miguu wala hawatazimia.

## *Ni ashiki ndani yako pekee itakayo washa ashiki za wengine*

Sheria ya Mungu inatangaza kwamba kila mbegu hutoa mbegu nyingi zaidi za aina yake. Ukitaka mahindi, lazima upande mahindi. Ukitaka kuvuna ngano, lazima upande ngano.hi sio sheria ya kiasili pekee lakini ni ya kiroho pia. Mungu hadhihakiwi. Chochote mwanadamu anapanda, ndicho atakachovuna.

Kushiriki ukweli wa Neno la Mungu na wengine utawasha ashiki katika maisha yao, kama utashikilia himizo la kweli na una ashiki kuhusu ukweli unao shiriki. Mambo usemayo hayatawasha moto ndani ya wengine yasipo waka ndani yako kwanza. Labda hii ni njia moja ya kubainisha ujumbe ambao Mungu ametupea tushiriki na wengine. Una ashiki kuhusu nini? Shawishi zako za kweli ni gani? Ni ujumbe mgani Mungu amekupatia unao weza kubadilisha maisha ya watu? Usiwahi kuwa na uoga kushiriki shawishi zako na ashiki ambazo Mungu amekupa.

## *Ombi la leo*

Baba, naamini na nimeshawishika kwa ukweli wa Neno Lako. Nina imani, Bwana, najua kwamba ushuhuda wangu utabadilisha maisha ya wale wanao nisikiza mimi. Nachagua ,Bwana, kuwachilia imani yangu, ushawishi wangu, ashiki yangu na ari yangu. Amina.

## *Maandiko ya leo*

Yohana 2:17; Wanafunzi wake wakakumbuka kwamba Maandiko yasema: "Upendo wangu kwa nyumba yako waniua."

Wagalatia 6:7; Msidanganyike; Mungu hafanyiwi dhihaka. Alichopanda mtu ndicho atakachovuna.

Zaburi 69:9; maana wivu wa nyumba Yako umenila, nalaumu zao wanao kulaumu zimenipata.

# ***Mvua kuu huanza na mawingu madogo***

1 wafalme 18:44; ikawa mara ya saba akasema, tazama, wingu linatoka katika bahari, nalo ni ndogo kama mkono wa mtu. Akanena, enenda umwambie Ahabu, tandika, ushuke, mvua isikuzuie. Ikawa, mda si mda, mbingu zikawa nyeusi kwa mawingu na upepo, ikanyesha mvua nyingi. Ahabu akapanda garini, akaenda zake Yezreeli. Mkono wa Bwana ulikuwa juu ya Elia; akajikaza viuno, akapiga mbio mbele ya Ahabu mpaka kuingia Yezreeli.

Kazi kuu za Mungu huanza katika maisha ya watu wake kwa kila njia ndogo na isiyokuwa ya maana. Mti mkubwa wa mkuyu una asili yake katika chembe ndogo ya mbegu. Je, Mungu ana anza nini katika maisha yako leo? Katika wakati wa Mungu, ata anza kazi Yake kubwa katika maisha yako kupitia kitu kidogo…inaweza anza leo.

*Ombi la leo*

Baba, ahsante, maana unamaliza kazi nzuri uliyo anza ndani yangu. Je napatikana kwako ili unifinyange na unitengeneze katika mfano wa Mwanao umpendaye?. Tafadhali nipe makusudi ya maisha yangu na Unisaidie kuheshimu baraka ndogo ulizo nipa leo.

*Maandiko ya leo*

Mathayo mtakatifu 13:31-32; Yesu akawaambia watu mfano mwingine: "Ufalme wa mbinguni unafanana na mbegu ya haradali aliyotwaa mtu mmoja, akaipanda katika shamba lake. Yenyewe ni ndogo kuliko mbegu zote, lakini ikishaota huwa kubwa kuliko mimea yote. Hukua ikawa mti, na ndege wa angani huja na kujenga viota katika matawi yake."

Luka Mtakatifu 17:6; Naye Bwana akajibu, "Kama imani yenu ingekuwa ndogo hata kama chembe ndogo ya haradali, mngeweza kuuambia mti huu wa mkuyu: `Ng`oka ukajipandikize baharini`, nao ungewatii.

## ***Mabadiliko katika mtazamo yanaweza kutoa madiliko katika viwango***

Mara kwa mara tunasikia, “mtazamo ni kila kitu.” La hakikisho ni kwamba, mabadiliko katika mtazamo yanaweza badilisha maisha yetu. Mtazamo ni baadhi ya mambo katika maisha ambayo tunaweza kudhibiti. Mtazamo wetu unatokana na tunachosikia, tunacho ona ama, tunachopitia. Kisha, tunakuza mawazo kutokana na haya mambo. Mawazo yana nguvu. Yale tunayowazia yana athiri vile tulivyo, tunavyosema na tunavyotenda.mtazamo wetu, hugusia sehemu zote za muhimu maishani mwetu: jamii zetu, kanisa letu na watu wengine.

Nikitambua mtazamo unaohitaji kubadilishwa ndani yangu, kuna matumaini. Njia ya muhimu ya kipekee kubadilisha mtazamo mbaya ni kumfanya Yesu Kristo Bwana wa maisha yangu na kufanya upya kujitolea kwangu kwa kila siku. “ hata imekuwa mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya; ya kale yamepita, tazama yamekuwa mapya.” (2 wakorintho 5:17) kwa kujitolea kwangu kwa mtazamo bora, naweza songeza milima. Aidha mtazamo wangu ni wa kinyume, niwakukubaliana, ama hapo katikati, ni kiwa na hiari kwa upande

wangu Mungu ana uwezo wa kubadilisha maisha yangu na kufanya yapae kwa viwango vingine vya ufanisi na utele.

*Ombi la leo*

Mungu, niliumbwa kwa maumbile yako na nimepewa uhuru wa mapenzi yangu kuchagua kile kitakacho kaa kwenye mawazo yangu. Nachagua kuangalia mambo kupitia Wewe na kutoa maisha yangu kwa mapenzi Yako.

*Maandiko ya leo*

Warumi 12:2; Msiige mitindo ya ulimwengu huu, bali Mungu afanye mabadiliko ndani yenu kwa kuzigeuza fikira zenu. Hapo ndipo mtakapoweza kuyajua mapenzi ya Mungu, kutambua jambo lililo jema, linalompendeza na kamilifu.

## ***Kwa sababu mambo ni mabaya haimanishi hatuwezi kuyafanya yawe mabaya zaidi***

Mtume Thomas Aquinas akasema, “ tenda, lakini usizidishe.” Mawaidha haya ni ushauri mzuri na unastahili kuangaliwa. Maisha hutupatia fursa nyingi za kuzidisha kiwango kwa misukumo ya maisha, hali, na mazingara yanayoletwa kwetu. Haijalishi ni mbaya kiasi gani sasa, niamini mimi, unaweza kuifanya ikawa mbaya zaidi.

Usijiruhusu mwenyewe kwa starehe za kuzidisha kutokana na mwili ama unaweza kuchukuwa hali isiyodumu na uifanye ya kudumu. Milima yaweza kuwa vijibonde vidogo kama tunaweza kutenda inavyostahili mbele ya shida zetu. Sio unachopitia kinachojalisha zaidi, ila ni vile unavyopitia. Tengeneza mapito yako ya kutoka katika shida zako lakini sio kuingia katika shina.

*Ombi la leo*

Yesu, nakutangaza wewe leo kama chanzo cha ushindi wangu. Mimi ni mshindi kupitia damu ya Mwanakondoo na ushuhuda wangu. Shida zikikuja, neema na rehema Zako zitaniwezesha mimi. Nasikia sauti Yako inipeyao hekima na kunizuia kufanya hali zangu ngumu kuwa mbaya zaidi.

*Maandiko ya leo*

2Timotheo 3:11; udhalimu na mateso yangu. Unayajua mambo yaliyonipata huko Antiokia, Ikonio na Lustra. Nilivumilia udhalimu mkubwa mno! Lakini Bwana aliniokoa katika mambo hayo yote.

1 Petro 5:8 Muwe macho; kesheni! Maana adui yenu, Ibilisi, huzungukazunguka kama simba angurumaye akitafuta mawindo

## ***Hadithi ya maisha yako haijakwisha, lakini itaandikwa na uamuzi utakao ufanya siku zako za usoni***

Maisha ni maandishi ambayo ni Mungu pakee aweza kuandika. Hadithi inaelezwa kupitia miaka na kila uamuzi kuanzia sura mpya. Hadithi ya maisha yetu haiishi na mwisho na makosa mabaya tuliyo yafanya. Maisha ya Petro hayakuisha na yeye akimkataa Kristo wala mwisho wa Daudi kukumbukwa kama muuaji wa rafiki yake wa karibu.

Kila siku Mungu anatupatia fursa ya kuchagua mapenzi yake kwa maisha yetu. Siku moja wengine wataelezea hadithi ya maisha yako kulingana na utakapomalizia sio utakapo anzia. Anza kufanya uamuzi wa sawa leo na utafute neema ya Mungu kushida, kudumu, na kupita uamuzi wako mbaya.hadithi ya maisha yako haijakwisha ila itaandikwa na uamuzi unaoufanya siku zako za usoni

*Ombi la leo*

Baba,nisaidie kutumia siku zangu zilizopita kama mafunzo. Bwana nakuuliza neema Yako ili nifanye maadalizi ya kufaa na uamuzi kwa siku zangu za usoni na za wapendwa wangu.eleza mapenzi Yako katika sura baada ya sura ya maisha yangu na uamuzi baada ya mwingine.

*Maandiko ya leo*

Wafilipi 3:13; ndugu, sijidhanii nafsi yangu kwamba ni kwisha kushika; ila natenda neno moja tu; nikiyasahau yaliyomo nyuma nikiyachuchumilia yaliyo mbele. Nakaza mwendo, niifikilie mede ya dhawabu ya mwito mkuu wa Mungu katika Kristo Yesu.

Isaya 43:19; tazama, nitatenda neno jipya; sasa litachipuka; je! Hamtalijua sasa? Nitafanya njia hata jangwani na mito ya maji nyikani.

## ***Sauti za halali na zisizokuwa za halali za viongozi...zote zina ushawishi.***

Yesu alifananisha uongozi na utu. Alielekeza watu wenye mawazo, wenye mwelekezo, kuelekea kwenye ukweli na kuwaonyesha njia ya upendo, msamaha, na maisha ya umilele. Pahali pazuri kuanzia kwa kuelezea uongozi ni kwa Yesu. Sauti ya uongozi wa ukweli inajumuisha huruma, kuwezesha, kuhubiri, na kuzalisha Ufalme.

Watu wengi wana ushawishi kwa wengine na hujaribu kuwaongoza bila kuwa walifikia kiwango chao cha uongozi kwa njia halali. Utofauti kati ya kiongozi halali na asiyekuwa halali haiwezi kuonekana kwa ushawishi walionao ila kwa jinsi waliupata uongozi ule. Ni muhimu kwetu kufuata sauti halali ya uongozi iliyotiwa nguvu na Mungu na iliyowekwa kwa utaratibu ambao umetambulika na kukubalika. Jihadhali na manabii ambao wamejiteua.

*Ombi la leo*

Baba, nipe nguvu na neema kuzijua vipawa ambazo ziko ndani yangu na uruhusu vipawa hizi zifanye kazi kupitia kwangu kwa upendo na nguvu Zako. Nisaidie nitambue sauti zinazo nishawishi mimi.

*Maandiko ya leo*

1 Wakorintho 9:26; Ndivyo basi, ninavyopiga mbio nikiwa na nia ya kushinda; ndivyo ninavyopigana, na si kama bondia anayetupa ngumi zake hewani.

Yakobo 3:1; Ndugu zangu, wengi wenu msiwe walimu. Kama mjuavyo, sisi walimu tutapata hukumu kubwa zaidi kuliko wengine.

## ***Mungu hana wajukuu***

Mungu ametengeneza jamii Yake iwe na waume, wake, wavulana, na wasichana wa umri, kabila,mataifa yote kila mmoja akiwa mtoto Wake na Yeye akiwa baba yao wote. Kila mtu amezaliwa tena katika uhusiano wake. Mungu hana wajukuu, ni watoto pekee. Ukweli kuwa mama yako ni mwana wa Mungu haukupei uhusiano na Yeye. Kila mtu lazima azaliwe tena.

Ni kwa sababu hii lazima tufanyike mashahidi wakati wote ili wengine wamjue Baba yetu kama Baba yao pia. Nimetafuta Neno nikiangalia tumaini lolote ya kumfanya mtu asiye mjua Yesu kama mwokozi wa

maisha yake bado anaweza kukaribishwa mbinguni…sijapata lolote. Lazima uzaliwe mara ya pili.

## *Ombi la leo*

Mpenzi Bwana, nifunze zaidi kuhusu uhusiano nilio nao na Wewe kama Baba yangu. Nipe ashiki ninayohitaji kuwaongoza wengine kwako Wewe. Niweke katika jamii Yako kama inavyokupendeza Wewe, katika jina la Yesu.Amina.

## *Maandiko ya leo*

Warumi 8:16; Naye Roho mwenyewe anajiunga na roho zetu na kuthibitisha kwamba sisi ni watoto wa Mungu.

Wagalatia 3:26; Kwa njia ya imani, ninyi nyote mmekuwa watoto wa Mungu katika kuungana na Kristo.

1 Yohana 5:2; Hivi ndivyo tunavyojua kwamba tunawapenda watoto wa Mungu: Kwa kumpenda Mungu na kuzitii amri zake;

## ***Watu wengine wameridhika kwa viwango vya chini kuliko kiwango cha bora kwao na umuhimu wao kwa Mungu kwa sababu hawana maono kuliko shani yao.***

“ tumesikia kuwahusu. Tunajua kwamba Mungu yuko pamoja na nyinyi, na kwamba mtashinda.” Hivi ndivyo Rahabu aliwaeleza wageni wake wawili siku hiyo. Alijua ya kwamba hawa wawili walikuwa maskouti, waliotumwa na kikundi cha uvamizi cha nguvu ambacho hakijawahi pingwa na mtu. Pia, alifahamu sababu ya ushindi wao ni Mungu alikuwa kwa upande wao. Maisha ya Rahabu, mji wake, yalikuwa yanaenda kubadilika hata milele. Angefanya nini? Akawapa wana wa Israeli usaidizi wake, kisha akawaomba wamkumbuke yeye na jamii yake watakapowaingilia. Kwa vile Rahabu alikuwa na maono zaidi ya hali yake ya saa hiyo,shani yake ilikuwa imeanza tu.

Maisha ni ya kustajabisha , kila wakati yakibadilika. Wakati mwingine ni mazuri, wakati mwingine ni mabaya, mabadiliko ni sehemu ya safari. Kama Rahabu, tunahitaji kuwa na maono zaidi ya hali yetu ya sasa. Hii inaanza tunapopeana maisha yetu kwa Mungu na kupiga hatua na mpango Wake wa maisha yetu. Mabadiliko yanakuja na hatupaswi kuwa na uoga tunapojiunganisha na mpango wa Mungu.

*Ombi la leo*

Baba, najua naweza kukuamini Wewe na siku zangu za usoni.tafadhali nionyeshe jinsi ya kujiandaa kwa sababu ya shani yangu Uliyonayo, na unionyeshe jinsi ya kuunganisha maisha yangu na kazi Yako. Tafadhali nipe maono zaidi ya shani yangu ya sasa.

*Maandiko ya leo*

Waebrania 11:31; Kwa imani Rahabu aliyekuwa malaya hakuangamia pamoja na wale waliomwasi Mungu, kwa sababu aliwakaribisha wale wapelelezi.

Mithali 23:17; moyo wako usiwahusudu wenye dhambi; Bali mche Bwana mchana kutwa. Maana kila shaka iko thawabu; na tumaini lako halitabadilika.

## ***Huenda Mungu hawezi kukupea wewe kile ambacho hawezi kupeana kupita kwako***

Bahari iliyokufa kule Israeli ni pahali pa kushangaza. Iko pahali pa chini sana duniani ambapo hapajafunikwa na maji. Sababu inayofanya iitwe bahari iliyo kufa ni kiwango kingi cha maji yenye madini ambacho hakiruhusu maisha kuendelea pale. Ni ajabu kusimama kado ya bahari hii ya kupendeza naugundue kuwa hakuna samaki, ama maisha ya majini ndani yake na pia hakuna ndege wanaokunywa haya maji. Kiwango cha madini ni kingi na maji yana kina kwamba mtu aweza kuelea juu bila juhudi kubwa.

Mwili wa maji umekufa kwa sababu moja na sababu moja pekee: maji safi yaliyo jaa uhai yanayotiririka kutoka mto Yorodani na vijito vyake vingi hayana pahali pa kutokezea. Kinachotiririka kwenye bahari iliyokufa hakiwezi kutiririka kupitia bahari iliyo kufa. Kwa hivyo, bahari iliyokufa, kila wakati inachukua ndani bila kutoa nje, hiyo inautajiri mwingi katika madini lakini imekufa kabisa. Usiwe bahari ambayo imekufa.

*Ombi la leo*

Baba, tafadhali fanya roho yangu iwe kama Yako. Nionyeshe jinsi yakufanyika mtoaji sio kila wakati wakupokea. Ongezea ndani yangu hamu ya kutumia kila Unachonipea mimi kuwekezea ndani ya maisha ya wengine.

*Maandiko ya leo*

Mathayo mtakatifu 25:29; Maana, aliye na kitu atapewa na kuzidishiwa. Lakini yule asiye na kitu, hata kile alicho nacho kitachukuliwa.

Mithali 11:24; Kuna atawanyaye, lakini huongezewa zaidi; kuna azuiaye isivyo haki, lakini huelekea uhitaji.

Mwanzo12;2; akasema, umchukue mwanao, mwana wako wa pekee, umpendaye Isaka ukaende zako mpaka nchi ya Moria, ukamtoe sadaka ya kuteketezwa huku juu yam lima moja wapo nitakaokuambia.

## *Mungu hatawahi choka kwa kutusaidia sisi tusimkosee Yeye*

Mungu hatawahi choka kwa kutusaidia tusimkosee Yeye, mradi hilo ndilo lengo letu. Kama Yesu katika Shamba la Gethsamane, akiomba katika lisaa lake la hitaji, hata sisi mara kwa mara hujikuta tukitafuta msaada wa Mungu wakati wetu wa majaribu na matatizo. Yesu aliomba atengwe na msalaba na uchungu aliokuwa ameteuliwa kupitia. Hata hivyo, maombi yake matatu yote yalikamilika na sala , "Sio mapenzi yangu, ila Yako yafanyike."

Mungu ni msaada wetu wa karibu wakati wote na hatatuacha wala kututenga. Amesema kuwa twaweza kusema kwa ujasiri, "Bwana ni Msaada wangu, nimwogope nani?" Kwa hivyo, simama na ukweli wa Neno la Mungu na kwa uhakika ukiri ukweli kwamba Mungu hatakosa kamwe kutusaidia.

*Ombi la leo*

Bwana, nataka kukupendeza Wewe kwa yote nifanyayo. Wakati matatizo, majaribu na mitihani ya maisha inanisonga, sikia kilio changu, na unikomboe na maadui wangu wote ili nisiwahi kukukosea Wewe. Hili ndilo shauku la moyo wangu, Ewe Bwana, kuwa mapenzi Yako, wala sio yangu, yatatendeka.

*Maandiko ya leo*

Zaburi 119:32; moyoni mwangu nimeliweka neno Lako, nisije nikakutenda dhambi.

Zaburi 27:13; naamini ya kuwa nitauona wema wa Bwana katika nchi ya walio hai.

Waebrania 13:5-6; Msiwe watu wa kupenda fedha; toshekeni na vile vitu mlivyo navyo. Mungu mwenyewe amesema: "Sitakuacha kamwe, wala sitakutupa." Ndiyo maana tunathubutu kusema: "Bwana ndiye msaada wangu, sitaogopa. Binadamu atanifanya nini?"

## ***Dhambi haina mipaka***

Hadithi ya Balamu katika Hesabu 22 hadi 31 hudhihirisha kuendelea kwa dhambi. Ikiwachiliwa yenyewe, dhambi haifanyiki bora ila mbaya zaidi. Kulingana na Agano Jipya, dhambi ya Balamu ilianza kama kosa kwa upande wake. Bila kuangaliwa, kuchangwa moto,na bila kubadilishwa Balamu aliendelea kupuuza himizo na akapea nafasi katika maisha yake dhambi kuota na kukua.

Hatimaye, dhambi ikachukua usimamizi wa maisha ya Balamu, na mwishowe, ikamgharimu huduma na maisha yake. Dhambi haijui mipaka yoyote. Hatuwezi achilia dhambi kuchukua nafasi yoyote maishani mwetu. Sio kwa mawazo yetu, sio kwa mipango yetu, na sio kwa matendo yetu. Dhambi itaangamiza vitu tunavyoipea na vitu tusivyoipea.

### *Ombi la leo*

Mungu, Yesu alikufa msalabani Kalivari kuondoa dhambi zangu. Nakushukuru kwa msamaha ambao Umenipatia kupitia damu Yake iliyomwagika. Ni nathiri yangu kutokubali dhambi kupata mizizi yoyote ama kutoa matunda yoyote maishani mwangu. Nitajichunguza, nijichange moto, na nibadilike kama ninavyopaswa. Nisaidie, Ewe Mungu.

### *Maandiko ya leo*

Yuda 1:11; Ole wao! Watu hao wamefuata mwenendo uleule wa Kaini. Kwa ajili ya fedha, wamejiingiza katika mkosi uleule wa Baalamu. Wameasi kama Kora alivyoasi na wameangamizwa kama yeye alivyoangamizwa.

Warumi 6:12; Kwa hiyo, dhambi isiitawale tena miili yenu ambayo hufa, na hivyo kuzitii tamaa zake.

Yakobo 1:15; Tamaa ikiiva huzaa dhambi; nayo dhambi ikikomaa huzaa kifo.

**Dhambi itakupeleka mbele zaidi kuliko ulivyotaka kuenda, ikuweke zaidi ya muda uliotaka kukaa, na ikugharimu pesa zaidi ya zile ulitaka kulipa.**

Hadithi ya Balamu inaendelea katika kitabu cha Hesabu na kuonyesha Balamu akiendelea zaidi katika dhambi. Kwanza alipea nafasi fikira ya dhambi. Hata hivyo, dhambi ikakuwa ndani ya maisha ya Balamu mpaka kiwango ambapo haikuwa makosa tena, sio kutojua tena. Sasa, ilifanyika mtindo wa maisha. Tamaa ya Balamu ikambeba zaidi. Ikiachwa bila kuangaliwa, kuchangwa moto, na kubadilishwa, dhambi itamuangamiza mtu hatua baada ya nyingine.

Dhambi itakupeleka mbali zaidi ya kule ulitaka kuenda, ikuweka pale zaidi muda uliotaka kukaa, na ikugharimu zaidi ya jinsi ulitaka kulipa. Hatutawachia dhambi nafasi kwa kusema, “hivyo ndivyo nilivyo”. makosa yakiachiliwa yenyewe yatafanyika mtindo wa maisha yetu, na njia za maisha ningumu kuchanga moto na kubadilisha kuzidi kosa la mara moja.

*Ombi la leo*

Baba, nisaidie nisichukue dhambi zangu kwa urahisi ama ni puuze himizo la Roho Mtakatifu anapotaka kuchunguza, kuchanga moto, na kubadilisha vile nilivyo. Nipe kuona na nguvu kuniepusha na dhambi. Ahsante, Baba.

*Maandiko ya leo*

2 Petro 2:15; Wameiacha njia iliyonyoka, wakapotoka na kuifuata njia aliyofuata Balaamu, mwana wa Beori, ambaye alipendelea kupata faida kwa kufanya udanganyifu,

Warumi 6:14; Maana, dhambi haitawatawala ninyi tena, kwani hamko chini ya Sheria, bali chini ya neema.

1 wakorintho 6:18; Jiepusheni kabisa na uzinzi. Dhambi nyingine zote hutendwa nje ya mwili lakini mzinzi hutenda dhambi dhidi ya mwili wake mwenyewe.

***Hatuangamii kwa dhambi zetu peke yetu ...tunachukua wengine nasi.***

Sura ya mwisho ya hadithi ya Balamu hudhihirisha mtu ambaye ameingia sana kwa dhambi kiasi cha kwamba hata amejindanganya mwenyewe. Ingawa hangewalaani wana wa Isiraeli, kwa kuogopa hasira ya Bwana, aliwaonyesha wengine hata hivyo, jinsi ya kupata ushindi dhidi ya wana wa Mungu. Kulingana na Ufunuo 2:14, dhambi za Balamu, zilizo anza kama makosa na kisha zikafanyika mtindo wa maisha, hatimaye zillikumbatiwa kama mafunzo. Balamu aliwafunza wengine jinsi ya kuweka kikwazo mbele ya wana wa Isiraeli.

Dhambi ikiruhusiwa kuendelea mkondo wote ndani ya maisha ya mtu, hufanya mtu huyu awabadilishe watu wengine wawe kama yeye waingie ndani ya  shimo la jehanamu. Jichunguze mwenyewe, jichange moto, na ubadilishe mtindo wako wa maisha leo. Usimpe shetani nafasi asije akakushinda wewe mwenyewe.

## *Ombi la leo*

Baba yangu, nisamehe kwa kuruhusu dhambi ipate nafasi yoyote ndani ya maisha yangu. Naomba uweze kuwakomboa wale nimeshawishi kimakosa kwa sababu ya dhambi zangu. Wacha wengine wanaosikiza na kunifuata wanifuate vile pekee ninavyokufuata Wewe. Amina

## *Maandiko ya leo*

Ufunuo 2:14: Lakini ninayo machache dhidi yako: baadhi yenu ni wafuasi wa Balaamu aliyemfundisha Balaki kuwatega wana wa Israeli wale vyakula vilivyotambikiwa sanamu za kufanya uzinzi.

1 wakorinitho 11:1; Niigeni mimi kama ninavyomwiga Kristo.

Yoshua 22:20; Je! Huyo Akani mwana wa Zera hakukosa katika vile vitu vilivyowekwa wakfu, na hasira ikawaangukia mkutano wote wa Israeli? Kisha mtu huyo hakuangamia peke yake katika uovu wa Israeli?

# ***Maisha ni mtihani... pita***

Majibu kwa majaribu magumu na mitihani ya maisha yote yameshughulikiwa katika Neno takatifu la Mungu. Mara nyingi tunahisi ya kwamba tunajaribiwa na mazingara na hali tunazokumbana nazo. Maisha huenda yakawa magumu wakati Fulani na wengine wetu sio wazuri kwa mitihani.

Hata hivyo, kuna habari njema! Sio kila mtihani ni kitabu kilichowazi ambacho tumepewa majibu katika Bibilia, pia tumetiwa moyo kuuliza maswali na kupata usaidizi mwingine kutoka kwa waalimu wetu na wengine wengi ambao tayari wameshapitia mtihani huo. Kwa hivyo, usikate tamaa usipopita mtihani, utapata fursa ya kuufanya tena.

*Ombi la leo*

Baba, natambua kwamba Neno Lako halijaribu wala kuwatihani watoto Wako na maovu. Najua Wewe sio mwanzilishi wa uovu unao kuja kwangu. Wewe ni jibu la shida zangu zote. Nifunze Neno lako na unipatie fursa ya kufunza wengine katika mitihani yao maishani pia. Ahsante kwa Bibilia.

*Maandiko ya leo*

2 Timotheo 3:16; Maandiko yote Matakatifu yameandikwa kwa uongozi wa Mungu, na yanafaa katika kufundishia ukweli, kuonya, kusahihisha makosa, na kuwaongoza watu waishi maisha adili,

Yakobo 1:13; Kama mtu akijaribiwa, asiseme: "Ninajaribiwa na Mungu." Maana Mungu hawezi kujaribiwa na uovu, wala yeye hamjaribu mtu yeyote.

## *Pengine idadi kubwa ya watu utakoa waathiri kwa Yesu, ni watu ambao bado haujakutana nao*

Kuna watu wengi ambao hatuwajui zaidi ya wale tumekutana nao. Hii inatuwezesha kuweka mtazamo ya kwamba kila wakati kuna uwezo katika siku zetu za usoni kuliko yale tumeshafanya.

Bila kutambua ni watu wangapi tumeshawahi kushuhudia kufikia hapo, twaweza kusisimuka kujua ya kwamba idadi kubwa ya watu ambao tutawahi waathiri kwa sababu ya Yesu ni watu ambao hata hatujawahi kukutana nao… labda ni watu ambao hawajazaliwa. Watu wana mhitaji Bwana na wanangoja kusikia …watu wengi wapya! Kutana na mtu mgeni leo.

*Ombi la leo*

Ningependa kuwa wakushinda nafsi kwako Mungu. Nifanye mvuvi wa watu na unionyeshe mashamba ya mavuno ambayo yameiva na

yameandaliwa juu yangu. Nisaidie nihifadhi mtazamo na nitambue ya kwamba watu wengi hawajapata kusikia kuhusu Yesu.

*Maandiko ya leo*

Yohana 4:35; Ninyi mwasema: `Bado miezi minne tu, na wakati wa mavuno utafika!` Lakini mimi nawaambieni, yatazameni mashamba; mazao yako tayari kuvunwa

Mathayo mtakatifu 4:19;  Basi, akawaambia, "Nifuateni, nami nitawafanya ninyi wavuvi wa watu."

Luka mtakatifu 10:2; Akawaambia, " Mavuno ni mengi, lakini wavunaji ni wachache. Kwa hivyo, mwombeni mwenye shamba atume wavunaji shambani mwake.

## *Pale Tunapoweka mipaka na Mungu ndipo anapoinulia mtu mwingine*

Mungu anampango na atafaulu. Ijapokuwa hapendelei, anaweza kufanya bila usaidizi wetu. Yeye anampango. Atafaulu na anatupatia fursa ya kuhusika. Hata hivyo kama kizazi cha Israeli kilichotoka Misri, ijapokuwa hawengeufuata mpango wa Mungu na kuchukua nchi ya ahadi, Yeye hakuwacha mpango Wake… alipata mtu mwingine ambaye angemfuata.

Esta aliambiwa na Moredikai kwamba kama hangeenda zaidi ya hofu zake na afanye kile Mungu alimuita yeye kufanya,  kwamba Mungu angemuinua mtu mwingine kufanya jambo lile, ila yeye na jamii yake wangepoteza.  Usichore misitari kwa mchanga na Mungu na ufikirie ina maana yoyote Kwake. Pale tunapoweka mipaka na Mungu, ndipo anapoinulia mtu mwingine aendelee zaidi yetu, na sana sana wao huendelea hata bila sisi.

*Ombi la leo*

Nakushukuru Ewe Mungu, kwa kunihusisha kwa mpango Wako. Nataka kuyafanya Mapenzi Yako yote kuhusu maisha yangu. Jukumu lolote, gharama yoyote, nitakufuata mpaka mwisho.

*Maandiko ya leo*

Matendo ya Mitume 20:24; Lakini, siuthamini uhai wangu kuwa ni kitu sana kwangu. Nataka tu nikamilishe ule utume wangu na kumaliza ile kazi aliyonipa Bwana Yesu niifanye, yaani nitangaze Habari Njema ya neema ya Mungu.

2 Timotheo 4:7; Nimefanya bidii katika mashindano, nimemaliza safari yote na imani nimeitunza.

Hesabu 14:24; lakini mtumishi wangu Kalebu, kwa kuwa alikuwa na nyingine ndani yake naye ameniandama kwa moyo wote, naye nitamleta yeye katika nchi hiyo aliyoingia; na uzao wake wataimiliki.